

# Chanjo ya COVID-19

## Chanjo ni nini?

Chanjo ni aina ya dawa. Inakuja kwenye sindano au shuti.

## Chanjo hufanya nini?

Kupata chanjo hukuepushana na kuugua. Kuna aina tofauti za chanjo za maradhi au magonjwa tofauti.

## Je, chanjo ni salama?

Ndiyo. Madaktari na wanasyansi hufanya kazi kwa bidii kuhakikisha chanjo ni salama. Chanjo tu ambazo ni salama ndizo zinazoidhinishwa kutumiwa nchini Kanada. Usalama wa chanjo hukaguliwa mara nyingi.

## Je, kuna chanjo ya COVID-19?

Ndiyo, kuna chanjo mpya chache za COVID-19.

## Je, chanjo za COVID-19 ni salama?

### Zilitengenezwa haraka sana.

Ndiyo. Madaktari na wanasyansi walifanya kazi kwa bidii kuhakikisha chanjo za COVID-19 ziko salama. Chanjo tu ambazo ni salama ndizo zinazoidhinishwa kutumiwa nchini Kanada. Usalama wa chanjo hukaguliwa mara nyingi.

## Je, ninaweza kuambukizwa COVID-19 kuitia chanjo?

La. Huwezi kuambukizwa COVID-19 kuitia chanjo. Chanjo husaidia mwili wako kutambua na kupambana na COVID-19.

## Je, kuna athari mbaya za chanjo ya COVID-19?

Baada ya kupata chanjo, huenda ukaathirika. Mkono wako unaweza kuwa na uchungu mahali ulipodungwa sindano. Huenda ukajihisi mchovu au mwenye joto jingi. Hii inamaanisha mwili wako unakubali chanjo. Athari hizi zinaweza kukaa kwa siku chache.

Watu wengine wanaweza kuwa na mizio wa chanjo. Watu wanaweza kuwa na athari mbaya zaidi. Athari hizi kali ni nadra.

**Unaweza pia kutembelea  
[manitoba.ca/COVID19/vaccine](https://manitoba.ca/COVID19/vaccine) ili upate maelezo.**

## Je, ikiwa dalili zangu zitakaa zaidi ya siku chache?

Huenda ulikuwa umeambukizwa virusi kabla ya kupata chanjo. Ikiwa dalili zako zitakaa zaidi ya siku moja au mbili, huenda umeanza kuugua. Unapaswa kujitenga (jiepushe na watu wengine) na upimwe COVID-19.

## Je, ni nani atapata chanjo kwanza?

Madaktari, wauguzi na watoa huduma wengine wa afya wanapata chanjo kwanza kwenye mkoa wa Manitoba.

Watu wale wengine wa kupata chanjo kwanza ni watu ambao wanaweza kuugua sana. Hii inajumuisha watu wazee na watu wa Kiasili.

## Ninaweza kupata chanjo lini?

Inachukua muda kutengeneza chanjo ya kutosha kwa kila mtu. Watu tofauti watapata chanjo kwa nyakati tofauti. Serikali na wataalam wanashirikiana ili kufanya maamuzi hayo. Maelezo zaidi yatatumwa wakati ukifika wa watu kupata chanjo.

## Je, ni lazima niendelee kuvaav maski na kukaa mbali na watu wengine nikipata chanjo?

Ndiyo. Kuvaav maski na kutokaribiana na watu kutakusaidia kukulinda na kuwalinda wengine.

## Je, ninahitaji kulipia chanjo?

Chanjo inatolewa bila malipo kwa watu wa Manitoba.

## Je, ni lazima nipate chanjo?

Chaguo ni lako ikiwa ungependa kupokea chanjo ya COVID-19. Sio lazima upokee chanjo.

Watu wengi wana maoni tofauti kuhusu chanjo hiyo. Maelezo mengine huenda si ya kweli.

Unaweza kuzungumza na watoa huduma za afya ili upate maelezo zaidi kuhusu chanjo. Watakupa maelezo sahihi.